# HURUMA YA MUNGU (SEHEMU YA 2 KATI YA 3): KUMBATIO LAKE LA JOTO

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Rehema, kama inavyodhihirika katika maisha ya dunia na Akhera.

**Aina:** Makala Imani za Uislamu Kuhusu Mwenyezi Mungu

**Na:** Imam Mufti

**Iliyochapishwa mnamo:** 03 Dec 2021

**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021

Rehema ya kimungu inafunika uwepo wote katika zizi lake, lenye kudumu milele. Mola Mlezi wa watu ni mwenye kuwarehemu, mwenye huruma. Jina la Mwenyezi Mungu, *Ar-Rahman*, linapendekeza rehema Yake ya upendo ni kipengele kinachobainisha nafsi Yake; utimilifu wa huruma zake hauna kikomo; bahari isiyo na mwisho isiyo na ufukwe. Ar-Razi, mmoja wa wasomi wa kiislamu wa kitambo aliandika, ‘Haiwezekani kwa viumbe kuwa na rehema zaidi kuliko Mwenyezi Mungu!’ Hakika Uislamu unafundisha kwamba Mungu ni mwenye huruma zaidi kwa mwanadamu kuliko mama yake mwenyewe.

Katika rehema nyingi za Mungu, Huteremsha mvua ili kuzalisha matunda kutoka kwenye bustani ili kuupa mwili wa mwanadamu. Nafsi pia inahitaji lishe nzuri ya kiroho kama vile mwili unavyohitaji chakula. Katika rehema zake nyingi, Mungu alituma manabii na wajumbe kwa wanadamu na kuwafunulia maandiko ili kutendeleza roho ya mwanadamu. Rehema ya Mwenyezi Mungu imejidhihirisha katika Torati ya Musa:

***"…Na katika maandiko yake mna uwongofu na rehema kwa wanao mwogopa Mola wao Mlezi." (Kurani 7:154)***

Na ufunuo wa Kurani:

***"…Hii (Kurani) ni hoja zinazo toka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu na rehema kwa watu wanao amini." (Kurani 7:203)***

Rehema haitolewi kwa sifa fulani za mababu. Huruma ya Kimungu inatolewa kwa kutenda kulingana na Neno la Mungu na kusikiliza kisomo chake:

***"Na hichi ni Kitabu tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa. Basi kifuateni, na mchenimngu, ili mrehemewe." (Kurani 6:155)***

***"Na isomwapo Kurani isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa." (Kurani 7:204)***

Rehema ni matokeo ya utiifu:

***"Na shikeni Swala, na toeni Zaka, na mt'iini Mtume, ili mpate kurehemewa." (Kurani 24:56)***

Rehema ya Mungu ni tumaini la mwanadamu. Kwa hiyo waumini wanamwomba Mwenyezi Mungu rehema yake.

***"Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unaye rehemu kuliko wote wanao rehemu!" (Kurani 21:83)***

Wanaomba rehema ya Mungu kwa uaminifu:

***"Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na utupe rehema itokayo kwako. Hakika Wewe ndiye Mpaji." (Kurani 3:8)***

Na wanawaombea rehema ya Mwenyezi Mungu wazazi wao:

***"…Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyo nilea utotoni.!" (Kurani 17:24)***

# Ugawaji wa Rehema za Mungu

Huruma ya kimungu inawafunga mikononi waaminifu na wasio na imani, watiifu na waasi, lakini katika maisha yajayo itawekwa akiba kwa ajili ya waaminifu. *Ar-Rahman* ni mwenye huruma kwa viumbe vyote duniani, lakini rehema yake imehifadhiwa kwa waaminifu katika maisha yajayo. *Ar-Raheem* atasambaza rehema zake kwa waumini siku ya kiama:

***"…Adhabu yangu nitamsibu nayo nimtakaye. Na rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wanao mchamngu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara zetu- Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili…." (Kurani 7:156-157)***

Ugawaji wa rehema za Mwenyezi Mungu umeelezewa na Mtume wa Uislamu:

***"Mwenyezi Mungu ameumba sehemu mia za rehema. Akaweka sehemu moja kati ya viumbe vyake kwa ajili ya kuhurumiana wao kwa wao. Mwenyezi Mungu amehifadhi sehemu tisini na tisa zilizosalia kwa ajili ya Siku ya Hukumu ili kuwafadhilisha waja Wake." (Saheeh Al-Bukhari, Saheeh Muslim, Al-Tirmidhi, na wengineo.)***

Sehemu ndogo tu ya rehema ya Mwenyezi Mungu inajaza mbingu na ardhi, wanadamu wanapendana, wanyama na ndege wanakunywa maji.

Pia, rehema ya Mungu ambayo itadhihirika Siku ya Hukumu ni kubwa kuliko yale tunayoyaona katika maisha haya, kama vile adhabu ya Mungu itakuwa kali zaidi kuliko ile tunayoipata hapa. Mtume wa Uislamu alielezea jinsi hizi sifa mbili tukufu zilivyokithiri:

***"Iwapo Muumini angejua ni adhabu gani aliyoiweka Mwenyezi Mungu, basi atakata tamaa na hakuna hata mmoja atakayetazamia kuingia Peponi. Kama kafiri angejua rehema nyingi za Mwenyezi Mungu, hakuna hata mmoja atakayekata tamaa kuifikia Pepo." (Saheeh Al-Bukhari, Saheeh Muslim, Al-Tirmidhi)***

Hata hivyo, katika mafundisho ya Kiislamu, rehema ya Mungu inapita hasira ya Mungu:

***"Hakika rehema yangu imepita adhabu yangu." (Saheeh Al-Bukhari, Saheeh Muslim)***

Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://webcache001.islamreligion.com/sw/articles/420/huruma-ya-mungu-sehemu-ya-2-kati-ya-3

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2026 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.